



CHAMA CHA WAHASIBU TANZANIA (TAA)

TAARIFA KWA WANACHAMA WITO KWA WANACHAMA KUSHIRIKI KATIKA KAMATI YA UCHAGUZI 2026

Tafadhali rejea kichwa cha Habari hapo juu.

Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA) kinawataarifu wanachama wake kuwa kinatarajia kufanya uchaguzi mkuu wa viongozi siku ya Jumamosi tarehe 17/10/2026 jijini Dar es Salaam katika Mkutano mkuu wa 43 wa mwaka.

Kutokana na taratibu za chama, chama kinatangaza nafasi tano ambazo ni mwenyekiti na wajumbe Wanne kuwa kwenye Kamati ya Uchaguzi.

Majukumu ya Kamati yatakuwa ni kupokea maombi ya waombaji wote, kuyachambua kutokana na Kanuni za Uchaguzi wa Chama na kupendekeza majina kwa wagombea katika nafasi ya Rais, Makamu wa Rais na Wajumbe wa Baraza la Uongozi.

Sifa za waombaji ni kama zifuatazo;

1. Awe Mwanachama hai wa TAA
2. Asiwe Mjumbe wa Baraza la Uongozi wa TAA
3. Awe na uzoefu katika chama si chini ya miaka 4
4. Mwenye uzoefu katika masuala ya utawala na uongozi
5. Ambae hajawahi kuwa na kashfa au tuhuma yoyote katika chama.

Elimu ya Wajumbe inaotakiwa ni ;

1. Mwenyekiti awe ni Mwanasheria na cheo cha kuanzia Mwandamizi na kuendelea
2. Wajumbe wote pia waoneshe kuwa wamewahi kushiriki katika kazi kama hii sehemu yoyote.

Kazi hii itakuwa ya siku tano tu ikiwemo siku ya uchaguzi tarehe 17/10/2026.

Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe ya Mtendaji Mkuu

ceo@taa.or.tz Cc winifrida.taa@gmail.com

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 04/09/2026 saa 10:00 jioni.

Imetolewa na,

Winifrida Ngaraguza,
AFISA MTENDAJI MKUU